



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI



TANGAZO LA MWALIKO WA WAANGALIZI WA NDANI WA UCHAGUZI  
KATIKA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE JIMBO LA ISMANI,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA NA MADIWANI KATIKA KATA 12  
ZA TANZANIA BARA

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kufanya uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Ismani lililopo Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Mkoa wa Iringa na Madiwani katika kata 12 za Tanzania Bara. Uchaguzi huo utafanyika siku ya Jumatatu tarehe 01 Juni, 2026 katika Jimbo tajwa na kata zifuatazo:-

Na.	Halmashauri	Kata
1.	Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni	Mzimuni
2.	Halmashauri ya Manispaa ya Kahama	Zongomera
3.	Halmashauri ya Mji Nzega	Itilo
4.	Halmashauri ya Mji Tarime	Ketare
5.	Halmashauri ya Mji Kasulu	Nyumbigwa
6.	Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi	Kala
7.	Halmashauri ya Wilaya ya Igunga	Ziba
8.	Halmashauri ya Wilaya ya Mlele	Kamsisi
9.	Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe	Nyamugali
10.	Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru	Namasakata
11.	Halmashauri ya Wilaya ya Chato	Bwongera
12.	Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti	Kibiti



Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 13(1) na (2) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inatoa mwaliko kwa waangalizi wa ndani wa uchaguzi wenye nia ya kuangalia uchaguzi.

Hivyo, kupitia tangazo hili, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inakaribisha maombi kutoka kwa taasisi na asasi za ndani zenye nia ya kuangalia uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Ismani na Madiwani katika kata 12 za Tanzania Bara kama zilivyoainishwa kwenye jedwali.

Taasisi na asasi zenye nia ya kuangalia uchaguzi huo ziwasilishe maombi kwa kutumia kiunganishi (*link*) kifuatacho: <https://ams.inec.go.tz>

Barua ya maombi itapaswa kuainisha mambo yafuatayo: -

- i. Anuani kamili ya taasisi au asasi husika.
- ii. Mahali ambapo taasisi au asasi husika inafanyia kazi (*physical address*).
- iii. Shughuli ambazo zinafanywa na taasisi au asasi husika kwa mujibu wa hati ya usajili.
- iv. Sehemu ambazo taasisi au asasi inapenda kwenda kuangalia uchaguzi.
- v. Idadi ya watu ambao taasisi au asasi itawatumia katika zoezi hilo pamoja na majina na taarifa zao binafsi.
- vi. Majina na namba za simu za viongozi watatu wa taasisi au asasi husika.
- vii. Ikiwa taasisi au asasi inahusisha viongozi ambao si raia wa Tanzania, viongozi wawili ambao taarifa zao zitawasilishwa ni lazima wawe Watanzania.
- viii. Nakala au kivuli cha hati ya usajili wa taasisi au asasi husika; na
- ix. Nakala au kivuli cha katiba ya taasisi au asasi husika.


Maombi hayo yatapokelewa kuanzia tarehe 21 Aprili, 2026 hadi tarehe 27 Aprili, 2026.

**Tume haitahusika na utoaji wa rasilimali fedha au rasilimali nyingine kwa ajili kugharamia zoezi la uangalizi wa uchaguzi kwa taasisi au asasi za kiraia zitakazopewa kibali.**



**Aidha, maombi yatakayotumwa kwa njia tofauti na mfumo ulioainishwa katika tangazo hili hayatafanyiwa kazi.**

Imetolewa leo tarehe 20 Aprili, 2026 na:



Kailima, R.K

MKURUGENZI WA UCHAGUZI

